JINA……**NAMBARI**……

SAHIHI YA MTAHINIWA ……

102/3 **TAREHE**: 26/07/13

KISWAHILI **SAA**: 5.30 – 8.00 mchana

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: SAA 2 ½

JULAI/AGOSTI 2013

RABAI DISTRICT
EXAMINATIONS BOARD

2013 MTIHANI WA MWIGO WILAYA YA RABAI

Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)

Maagizo

- Jibu maswali manne pekee
- Swali la kwanza ni la lazima
- Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; riwaya, Tamthilia, ushairi na Fasihi Simulizi.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- Watahiniwa wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa

Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SEHEMU A

HADITHI FUPI – na Ken Walibora na Said A. Mohamed

1. SWALI LA LAZIMA

Haayaa. Nini teena? Ebu niwaache. Kwani wadhani naataka kusaidiwa?.....

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza hali anazozipitia anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 4)

c) Eleza sifa za anayezungumuza maneno haya. (alama 4)

d) Kulitendeka nini hatimaye? (alama 8)

SEHEMU B. USHAIRI

Jibu swali la **pili** au la **tatu**

2. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. Naja sasa ni ndiyani, naja kwetu mzalendo
   Naja nirudi nyumbani, nilowekwa nako kando
   Kwetu mi nakutamani, kulo na mwingi uhondo
   Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani

2. Naja ni ndiyani naja, taratibu ndiwo mwendo
   Siku ambayo nangoja, kunyakuliya mdundo
   Iko karibu na kuja, siifanyi kishindo
   Nijaye ni ile nyundo, Misumari hadharani

3. Naja kwingine kuwapi, kulojaa langu pendo?
   Henda nende kwinginepi, sawa nako kwa muundo?
   Kaa kwingine anapi, ela kwenye lakwe gando?
   Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

4. Naja nije rudi papo, panigendeme mganso
   Ningaambwa kwetu hapo, kwanba kanuka uvundo
   Sitakwenda penginepo, ‘tarudi kuko kwa mwando
   Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani

5. Naja sitapakimbiya, ningambwa kuna vimondo
   'Takuja kuvilekeya, vinganijiya kwa rundo
   Nilipozawa ' tafiya, sikimbii kwenda kando
   Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani.

6. Naja hiwa 'mekomaa, kuzidi nilivyo mwando
   Tena nnajiandaa, kwa fikira na vitendo
   Kwetu nije kuifaa, na kuitiliya pondo
   Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani
   (sauti ya dhiki na abdilatif abdalla – 19 dec 1974)

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)

b) Andika maudhui yanayojitokeza katika ubeti wa 3 na wa 4. (alama 4)

c) Taja na utoe mifano ya tamathali za usemi mbili zinapatikana katika shairi hili. (alama 4)

d) Jadili umbo la shairi hili. (alama 4)

e) Mshairi ametumia uhuru wa kishairi kuendeleza utunzi wake. Taja moja ya uhuru wa kishairi uliotumika zaidi na uutolee mifano minne. (alama 4)

f) Andika ubeti wa sita (6) kwa lugha ya nathari. (alama 3)

3. Soma shairi hili na ujibu maswali yanayofuata

Shimo; - Ali Salim Zakwany

1. Mwambieni kibushuti, asiruke shimo lile
   Kimo chake kama goti, kwenda ng'ambu sifikile
   Mtu haoli bahati, akasahau umbile
   Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

2. Afanyayo ni hatari, sijitie mpulele
   Mambo yote ajasiri, shari asithibutile
   Mjalia watu kheri, shairi ni yake vivile
   Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

3. Asambe ndiyo busara, kutenda kitendo kile

   Itamuwia hasara, na madhara kama yale

   Mola mwingi wa subira, ajapo chomwa vidole

   Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

4. Licha na yeye nyadungo, chuya katika mchele
   Hata warefu ja pondo, hawatusi shimo lile
   Walojaribu kitendo, shimoni watumbukile
   Kila muwania mbele, na nyuma ' sisahawile

5. Nimefika kituoni, nasema mumuwasile
   Mfua maji ngamani, ili kwamba sizamile
   Chombo huungia mwambani, na nahodha ni yuyule
   Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (alama 1)

b) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 4)

c) Taja nautoe mifano ya tamathali za usemi mbili zinazopatikana katika shairi. (alama 4)

d) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)

e) Kwa kutoa mifano minne, eleza aina mojaya idhini ya kishairi iliyotumika zaidi katika shairi. (alama 4)

f) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (alama 3)

SEHEMU C: - RIWAYA

Said A. Mohamed: - Utengano

Jibu swali la 4 au la 5

4. Basi bwana huyo alikuwa maaluuni hasa alipojiona yeye ni mtu mkubwa……..

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Jadili sifa za mzungumziwa. (alama 6)

c) Anayerejelewa katika dondoo anasemekana alikuwa maluuni, Thibitisha kauli hii. (alama 10)

5. Utengano ni Riwaya iliyojaa maovu chungu nzima. Jadili hoja kumi kudhibitisha kauli hii. (alama 20)

SEHEMU D:- TAMTHILIA:

Mustahiki Meya na Timothy Arege

6. Jadili mbinu kumi alizotumia Mustahiki Meya kuendeleza uongozi wake dhalimu. (alama 20)

7. Jadili jinsi mbinu ya jazanda ilivyotumiwa na mwandishi kuiwasilisha kazi yake. (alama 20)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. Eleza sifa na umuhimu wa vipengele vifuatavyo

i. Lakabu (alama 10)

ii. Misimu (alama 10)

ANSWERS:

Order a copy of answers from www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs